

Pambazuko

Toleo Namba 0036

Jumatatu Mei 01-07, 2023



**Mappingamizi uraia
pacha kunguruma**

**Uk.
7**



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Hasira zionekane kwa mafisadi

MARA kadhaa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Majaliwa Kassim Majaliwa, amesikika akifoka, akionekana kukerwa na zaidi sana akithibitika kukasirika kwa matukio anayoyataja kuwa ni ubadhirifu na matumizi mabaya ya ama madaraka au fedha za walipakodi anapokuwa katika ziara za kukagua miradi ya maendeleo.

Ikumbukwe kuwa Septemba 8, mwaka jana, Majaliwa akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Tabora, alifika kwenye mradi wa ujenzi wa Chuo cha Veta Uyui, ambako alishangazwa kusikia kuwa kibanda cha mlinzi wa chuo hicho kimegharimu Sh. milioni 11.

Majaliwa alisema kwa muonekano, kibanda kile hakiwezi kuchukua kiasi hicho cha fedha alichoeleza na kwamba huenda kuna ubadhirifu umefanywa na kuamuru Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (Takukuru) kuwakamata na kuanza kuwachunguza wote waliohusika katika mchakato wa ujenzi huo.

Hiyo haikuwa mara ya kwanza kwa kiongozi huyo mkuu wa shughuli za serikali bungeni na mshauri -mtendaji wa karibu kabisa wa Rais Samia Suluhu Hassan, akifoka na kuamuru watendaji kukamatwa akiwa kwenye kadamnasi.

Pamoja na kwamba ni hatua nzuri kwa kiongozi wa juu kuonekana kukwera na yanayoendelea katika utekelezaji wa majukumu ya kuhakikisha maendeleo yanapatikana, bila kuwaibia wananchi kodi zao, bado kuna maeneo ambako

Rais Samia, Majaliwa na uongozi mzima wa serikali, wameshindwa kuonyesha hasira zao.

Maeneo hayo ni yale yanayothibitika katika vitabu vya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwamba kuna wizi mkubwa wa fedha za walipakodi wa Tanzania na hata zile zinazoletwa kwa njia ya mikopo na hata misaada kutoka nchi washirika wa maendeleo.

Kila mwaka CAG amekuwa akiibua madudu ya kutisha katika halmashauri, taasisi, wakala, kampuni na hata mashirika yanayoendeshwa na serikali moja kwa moja au kuwa na ubia, lakini hasira na sauti za kufoka hazisikiki kuwa kuu na zenye ukali kwa wahusika wanaoweza kuwekwa kwenye kundi la 'mapapa wezi.'

Pamoja na ubaya wa ubadhirifu mdogo, madhara yake yanaweza kuwa makubwa ikiwa yatajikusanya hata kufikia viwango vya ufisadi, ambao una ubaya mkubwa zaidi na kuwa na madhara yanayoumiza jamii pana zaidi.

Watanzania wanapenda kuona serikali ikichukua hatua kali zaidi kwa wote wanaofisidi nchi hii, hasa hao wanaobainika kukwapua fedha za maendeleo kwa manufaa binafsi, huku wakifanya mnyororo wa umasikini kuendelea kuwafunga wengi zaidi - na hata kupokewa na vizazi na vizazi.

Ikiwa hasira za serikali zitabaki kwa "vidagaa" tu, na mafisadi papa kuachwa, basi hata uchunguzi wa CAG na ushauri wake, hautakuwa na maana zaidi ya kujaza karatasi katika kabati za ofisi za wakubwa.

KUMBUKUMBU ...



Waasisi wanapokutana; kushoto ni Rais wa Zambia, Kenneth Kaunda, Rais wa Msumbiji, Samora Machel na Rais wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere. Wote hawa sasa ni marehemu. Hawa ni viongozi waliosaidia kupatikana kwa uhuru wa nchi zao na jirani, na wanakumbukwa zaidi kwa kuchochea pia ukombozi wa fikra. (Picha na Maktaba ya Pambazuko).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



“Mipango mingi ya serikali yetu (Tanzania), inashindwa kuendelea wala kuleta matokeo chanya na makubwa, kwa kuwa kila baada ya muda mfupi, inabadilika ama kuachwa kabisa kwa kuwa kila kiongozi, anayeingia madarakani, anakuwa na matamano yake binafsi na halazimiki kufuata ya mtangulizi wake. Hatufiki bila kuwa na dira itakayosimama bila kujali nani anaingia madarakani”

- Mchungaji Peter Msigwa, mbunge mstaafu.

Habari

TTB, Tanapa 'kupika' waandishi

Na Mwandishi WETU

BODI ya Utalii Tanzania (TTB) na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), yamewahakikishia waandishi wa habari kwamba wataendelea kutoa mafunzo zaidi kwa waandishi wa habari ili kupata fursa ya kutangaza vivutio vya utalii duniani.

Mkurugenzi Mkuu wa TTB, Damas Joseph Mfugale, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, wakati akifunga mafunzo kwa waandishi wa kidigitali, alisema bodi anyoiongoza, imedhamiria kushiriki kutoa mafunzo zaidi kwa wanahabari ili watangaze kuwepo kwa vivutio vya utalii.

Amesema ikiwa waandishi wa habari watakuwa na uelewa mpana juu ya vivutio vya utalii, ni rahisi zaidi kwao kuweka 'mabango' zaidi kwenye vyombo vya na kufikia idadi kubwa ya watalii wa ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

Mfugale alisema kuongezeka kwa idadi ya watalii, kuna akisi ongezeko la fedha kwenye Hazina ya serikali, hivyo kutoa mwanya kufanyika kwa shughuli kubwa za maendeleo kwa Watanzania.

Kamishna Mkuu wa Tanapa, William Simon Mwakilema akizungumza umuhimu kwa waandishi

kupata mafunzo kuhusu kuutangaza utalii wa Tanzania, alisema vyombo vya habari ni nyenzo muhimu kuhakikisha vivutio vya Tanzania vinapaswa kufahamika kwa watu wengi zaidi duniani ili wafike kushuhudia.

Mhifadhi Mwakilema aliwahakikishia waandishi wa habari kwamba Tanapa, itakuwa pamoja nao katika kusaidia kuwapa mafunzo kila inapojitokeza fursa ya kufanya hivyo, kwani bila wao



vivutio vitakosa maana ikiwa havitambuliki.

Ijumaa iliyopita, waandishi wa habari walioboea kutumia mifumo ya kidigitali Tanzania walipewa

mafunzo ya namna nzuri ya kuutangaza utalii wa nchi hiyo kupitia mitandao ya kijamii.

Mafunzo yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi na Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari Tanzania, (Tampa), yalikuwa na lengo kubwa la kuwapa mafunzo waandishi hao kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania kwa dunia.

Rais wa Tampa, Simon Mkina aliliambia gazeti la kidigitali la Pambazuko kwamba mafunzo hayo yalifanikiwa kwa kiasi kikubwa baada ya washiriki 45 kuhudhuria na kufundishwa namna ya kuandika na kutangaza vivutio vya Tanzania.

Waandishi hao walipewa mafunzo ya matumizi ya mitandao ya kijamii 'kupaisha' utalii wa Tanzania, mbinu za kufikia idadi kubwa ya wataji; na umuhimu wa teknolojia ya habari katika kukuza soko la utalii.

Mkina alisema kuwa mafunzo hayo yamaenza kwa waandishi wa Dar es Salaam, lakini yatasambazwa kwa mikoa mingine kadri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu na kwamba kuomba taasisi na kampuni za utalii kusaidia kusambaza elimu hiyo kupitia mafunzo yanayoratibiwa na Tampa.

Amesema kuwa mafunzo hayo yatawafikia waandishi kutoka kwa walimu wabobezi wa masuala ya utalii ambao ni wakufunzi wa Chuo cha Taifa cha Utalii, kilichopo Dar es Salaam pamoja na wataalamu wa masuala ya teknolojia ya habari kutoka vyuo vikuu.



Wakili ICC kuwania Makamu Rais TLS

Na Tryruckia MFINANGA

WAKILI pekee Mtanzania katika Mahakama ya Kimataifa dhidi ya Uhalifu (ICC), Revocatus Lubigili Kuuli, amejitosa kuwania nafasi ya kuwa Makamu wa Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS). Uchaguzi huo utafanyika Mei 12 mwaka huu.

Kuuli, ambaye ni muumini na mtetezi mkubwa wa haki za binadamu, utawala bora na uwajibikaji, amesema anawania nafasi hiyo kwa kuwa anapenda kuona mawakili wakijenga umoja wenye nguvu kubwa, wenye maslahi sawa kwa kila mwanachana na zaidi sana kuhakikisha utawala wa sheria unachukua mkondo wake.

Hivi sasa akiwa Wakili Mkuu wa Serikali Wizara ya Katiba na Sheria, anapenda zaidi kuona Tanzania yenye kuheshimu misingi ya utawala bora na kufuata sheria katika kutenda haki bila kujali dhamana ya mtu, hadhi, hali ya uchumi, jinsi na hata rangi.

Akizungumza na Pambazuko, Kuuli amesema anaamini wanachama wa chama hicho cha kitaaluma kwa wanasheria, watampa nafasi hiyo na kwamba atashirikiana nao kuipa nguvu zaidi TLS.

"TLS ni miongoni mwa vyama vya kitaaluma katika Afrika kilichojenga heshima kubwa kwa muda mrefu, sasa nimeona vyema nani niweke uwezo wangu wa kuongoza kwa kuwania nafasi ya makamu wa rais, ikiwa wanachama wenzangu watanipa ridhaa, kupitia sanduku la kura, nina imani sitawaangusha na nitahakikisha tunashirikiana kujenga TLS bora zaidi na yenye maslahi mapana kwa kila wanachama," amesema Kuuli.

Amesema mawakili wa Tanzania



Wakili Kuuli

hawajatumia nafasi zao kupata fursa za kujiua kimataifa, hivyo akipata nafasi atatumia uwezo wake kuhakikisha mawakili wenzake wengi zaidi wanapata mwanya wa kunufaika na nafasi za mawakili katika medani za kimataifa.

Kuuli, shabiki wa utawala bora, anasema msukumo wa kunai nafasi hiyo pia umetokana na uwezo wa watangulizi wake katika kuijenge TLS, hivyo anapenda kuongeza pale walipoishia – kwa kushirikiana na uongozi mpya na wanachama kuhakikisha heshima, hadhi na maslahi ya chama chao "hayachezewi" na yeyote.

"Endapo nitapata nafasi hii ninayoomba, wanachama wapate imani kwamba kamwe sitawaangusha, na ninaomba kwao kura za kutosha kufanikisha ili twende pamoja katika kukuza na kujenga wigo mpana na shirikishi wenye maslahi kwa kila mmoja," ameongeza Kuuli.

Kuuli amesema licha ya kuwa wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania na Mahakama Kuu ya Zanzibar, pia ni wakili mwanachama wa Chama cha Mawakili wa ICC (ICCBA) na Chama cha Mawakili wa Mahakama ya Umoja wa Mataifa (UN-IRMCT).

Habari

Mafuta, gesi zaidi ‘vyanukia’ Tanzania

Na Scovya MANASE

NEEMA za Tanzania zinaendelea kufunguka na huenda zikaongezeka zaidi baada ya kubainika kuwepo dalili zote za kupatikana kwa mafuta na gesi asilia katika Bonde la Eyasi Wembere.

Bonde hilo linalounganisha mikoa mitano; Arusha, Singida, Tabora, Shinyanga na Simiyu, linaonyesha kuwepo kwa viashiria vya kupatikana mafuta na gesi asilia.

Uchunguzi uliofanywa na Pambazuko unaonyesha kwamba sampuli zaidi ya 1,100 za miamba, udongo, mchanga majimaji na vimelea kadhaa zilizochotwa katika maeneo mbalimbali ya mkuza wa bonde hilo zinaonyesha kuwepo kwa mafuta na gesi asilia; nishati muhimu katika kukuza uchumi.

Sampuli hizo zimepelekwa maabara ya ALS iliyokuwa Houston, Texas, Marekani, inatarajia kutoa matokeo ya utafiti wake mwishoni mwa mwaka huu, 2023.

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), ambalo husimamia shughuli zote za utafiti wa nishati ya mafuta kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, ilianza kufanya utafiti wa mafuta ya petroli katika Bbonde la Eyasi Wembere kuanzia mwaka 2015.

Utafiti wa awali wa wataalamu wa TPDC – kwa kushirikiana na wengine kutoka nje ya Tanzania, ulihusisha uchorongaji wa visima vitatu vya utafiti vyenye urefu wa mita 300 kila kimoja na hivyo kufanya jumla ya mita 900 zilikazochorongwa katika bonde hilo.

Kisima namba moja kinachorongwa katika Kijiji cha Kining'nila Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, kisima namba 2 na 3 vinachorongwa katika wilaya za Meatu, Simiyu na Iramba, Singida.

Bonde la Eyasi Wembere limebainika kuwa na miamba tabaka mizuri ambayo inakusanya dalili za kuwepo kwa kiasi kikubwa cha mlundikano wa viashiria vya kuwepo mafuta na gesi asilia.

Pambazuko limepata taarifa kwamba



Mkurugenzi Mtendaji TPDC, Mussa Makame

utafiti wa awali ulihusisha utaalumu wa kurusha ndege maalum za utafiti ambazo hupiga picha jongefu na kuparaza nakala (scan) zinazobeba sampuli ndani ya ardhi na miamba.

Hadi sasa mita zilizochorongwa katika visima hivyo ni zaidi ya 200 kati ya 300 zinazopaswa kuchorongwa.

Meneja mradi wa utafutaji mafuta katika Bonde la Eyasi Wembere, Sindi Maduhu ameliambia Pambazuko kwamba dalili za kuwepo mafuta na gesi huthibitishwa kwa matokeo ya maabara na kazi zingine za kitaalamu, na kwamba huchukua muda mrefu kufikia kutangaza rasmi kuwepo kwa nishati hiyo.

Pambazuko limebaini kwamba zaidi ya Sh. 2,400,000,000 (bilioni 2.4) zilitumiwa na TPDC kuagiza, kutunza na kugharimia utafiti huo wa ndege maalum.

Pamoja na kwamba haikuthibitishwa ndege hiyo ilitoka nchi gani, lakini kampuni za utafiti zinazokodisha wataalamu na ndege kufanya kazi hizo ziko Marekani, Australia na Afrika Kusini.

Inatarajiwa kwamba mwishoni mwa mwaka kesho, 2024, huenda matokeo rasmi ya kuwepo kwa mafuta na gesi asilia katika Bonde la Eyasi Wembere.

Mappingamizi uraia pacha kunguruma

Na Tryruckia MFINANGA

MAHAKAMA Kuu, Masjala Kuu iliyoko Dar es Salaam, kesho – Aprili 2, itaanza kusikiliza mappingamizi matatu ya awali ambayo yamewasilishwa na upande wa Serikali ya Tanzania dhidi ya “wanadiaspora” ambao wanataka kuwepo kwa sheria ya uraia pacha.

Mappingamizi hayo ya awali ni kwamba waleta maombi hawakuweka sainei zao katika hati ya madai; kwamba madai yao yamekiuka masharti ya kifungu cha 4 cha sheria ya haki za msingi na wajibu kwa raia; na kwamba viapo vimeapwa nje ya Tanzania, lakini vimeshuhudiwa na wakili wa Tanzania.

Kesi hiyo ya Kikatiba namba 18 ya mwaka 2022 ilifunguliwa na Shaban Fundi, Patrick Nyelesa Nhgula, Restuta Kalemera, Nkole Muya, Emmanuel Emmanuel na Bashir Kassam dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Watanzania hao – kwa niaba ya wenzao, wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi hiyo, walifungua kesi ya kikatiba kupinga sheria inayozuia uraia pacha.

Viapo vya waleta maombi hawa vinaonyesha kwamba ni Watanzania kwa kuzaliwa walioondoka nchini na kwenda ughaibuni kwa nyakati tofauti tofauti hususani katika nchi za Marekani, Uingereza na Canada wanakoishi na kufanya kazi ambako pia walishapata uraia.

Wakili wa Watanzania hao, Peter Kibatata, amesema kuwa mappingamizi hayo yalitarajiwa kutoka upande wa serikali na kwamba timu yake imejipanga vyema kujibu hoja zote na kwamba “haoni hoja za msingi.”

Taratibu za Mahakama zinaonyesha kwamba baada ya kusikiliza mappingamizi hayo na hoja za waleta maombi, basi majaji hutoa uamuzi mdogo baada ya kuridhika na kuruhusu kesi ya msingi kuendelea. Mahakama inaweza kuyatupilia mbali mappingamizi ama kukubaliana nayo dhidi ya hoja za waleta maombi.



Wakili Peter Kibatata

Kimsingi, haya mappingamizi ya awali ni husimamisha kesi ya msingi kuendelea, lakini hayagusi mizizi ya kesi ya msingi, kwa kuwa huegemea zaidi katika “kughafirika kwa uwasilishaji wa shauri kisheria” na siyo kuharibu mwennendo wa kesi yenyewe.

Ikiwa mappingamizi yatakubalika, Mahakama hutoa muda kwa waleta maombi kuwasilisha upya – ikiwa itaonekana inafaa au kuamua kuendelea na kesi ya msingi.

Katika kesi hiyo wanaoimba mahakama itamke kuwa vifungu vya Sheria ya Uraia vinavyozuia uraia pacha ni batili wakidai kuwa vinakiuka haki zao za Kikatiba kwa kuwa vinawanyima haki ya asili “isiyonyang’anyika” yaani uraia wa kuzaliwa.

Katika viapo vyao wanaeleza kuwa wameathirika sana kitendo cha kunyimwa haki mbalimbali katika nchi yao waliyozaliwa kwa kuzingatia kwamba walipata uraia wa nchi hizo kwa sababu za kiuchumi na ustawi wa kijamii.

Miongoni mwa haki wanazozikosa nchini walikozaliwa ni pamoja na kutokuwa na haki ya kumiliki ardhini, kutokuchagua viongozi wala kushiriki kugombea nafasi ya umma katika uchaguzi nchini.

Rwanda

Bosi Alibaba kufundisha Rwanda

**Na Mwandishi WETU
Mashirika**

TAJIRI anayeshikilia nambari 26 kwenye orodha ya watu wenye ukwasi zaidi duniani, Jack Ma, raia wa China, ameahidi kuwa mkufunzi wa vyuo vikuu muda mwingi baada ya kustaafu “kusimamia” biashara zake.

Ma ambaye ni mmoja wa waanzilishi wa mtandao wa masoko wa Alibaba, amesema anarudi kwenye kazi anayoipenda zaidi; kufundisha darasani, ili kuzeeka “vizuri.”

“Sasa nimestaafu, na ninarudi kufundisha, kazi ambayo nimekuwa nikipenda tangu utoto wangu, naamini nitazeeka nayo vyema zaidi kuliko kukimbizana na fedha kila kukicha,” anasema Ma ambaye pia ni tajiri nambari tano nchini China, akiwa anamiliki dola za Marekani bilioni 23 (karibu Sh. trilioni 54)

Hivi sasa familia ya Bernard Arnault, ndiyo inaongoza kwa utajiri duniani ikifuatiwa na Elon Musk - kwa mujibu wa jarida la Forbes la Marekani.

Ma ambaye ni profesa, amepanga kuanza kufundisha katika vyuo vikuu vya Hong Kong, pia amethibitisha kwamba atakwenda Rwanda ambako atafundisha masomo ya biashara zaidi.

Akiwa Rwanda, Profesa Ma, atatumia muda mwingi kuwapa wanafunzi wake namna nzuri ya kuelekeza mafunzo ya biashara kwa vitendo na siyo nadharia pekee.

Inaelezwa kuwa Ma, akiwa ni shabiki na rafiki wa Rais wa Rwanda, Paul Kagame, atafundisha kwenye Chuo Kikuu cha Masuala ya Uongozi Afrika- African Leadership University (ALU) kilichopo mji mkuu wa nchi hiyo, Kigali.

Tayari chuo hicho kimetangaza katika tovuti yake kwamba Ma atakuwa miongoni mwa wakufunzi wanaotarajiwa kuanza kutoa mafunzo ya biashara



Rais Paul Kagame wa Rwanda akiwa na Jack Ma

na uongozi kwa ALU. Hata hivyo, haikuelezwa ni lini hasa ataanza kazi hiyo.

Mwanzilishi wa ALU, Dkt. Fred Swaniker, amesema vijana wengi wa Afrika wanaosoma katika chuo hicho, watapata nafasi ya kufundishwa na mmoja wa watu wenye mafanikio makubwa ya biashara duniani.

Historia ya Ma inaonyesha kwamba kabla ya kuanzisha Alibaba, alikuwa mwalimu, akifundisha Kiingereza, lakini baadaye aliamua kuacha na kuanza biashara ya kuzaa bidhaa mitandaoni.

Ma alianzia katika vyuo vikuu katika mji wa Hangzhou mashariki mwa Mkoa wa Zhejiang, China. Alanzisha kampuni ya Alibaba kutoka nyumbani kwake Hangzhou.

Miaka mitatu iliyopita, Ma, aliingia katika mgogoro na uongozi wa Serikali ya China, baada ya kuukosoa namna unavyoendesha nchi, akiutaja kujaa “amri zinazopitwa na wakati katika baadhi ya masuala yanayobadilika.” Uhusiano wake na watawala wa China siyo mzuri.

Alibaba, moja ya kampuni kubwa zaidi duniani, ilianzishwa na Ma mwaka 1999 na imeendelea kuimarika, licha ya yeye kuacha shughuli nyingi kwa watendaji. Yeye ni mwenyekiti asiyelazimika kufuatilia kila hatua ya utekelezaji wa majukumu ya Alibaba.



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mezani kwa Chahali

Tusirudi zama za mwanaharakati huru

MOJA ya kumbukumbu zisizopendeza za utawala wa John Magufuli ni kuibuka kwa “mwanahabari mmoja” aliyejiita “mwanaharakati huru.”

Japo hakuna sheria inayomkataza Mtanzania yeyote kuwa “msemaji wa serikali”, alichofanya huyo jamaa kiliathiri watu wengi, nami nikiwa mmoja wao.

Februari 28, 2018 itabaki kwenye kumbukumbu za Watanzania wengi, kwa sababu kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, mwanahabari huyo alitisha, alitisha mkutano na vyombo vya habari na kutoa tuhuma nzito dhidi ya Watanzania kadhaa, bila kuonyesha chembe ya hofu kwa kufanya hivyo.

Katika tukio hilo, “mwanahabari huyo” alitaja orodha ya watu tisa alioidai ni tishio kwa usalama wa taifa, na akawapachika jina la “watu hatari.”

Kwa bahati mbaya, hadi leo, zaidi ya miaka mitano baada ya tukio hilo, baadhi ya watu siyo tu huniita “mtu hatari,” bali pia baadhi yao waliamini “sumu” waliyolishwa na “mwanahabari huyo,” wanaendelea kunihisi vibaya.

Kwa bahati nzuri, tayari watu wawili waliorushiwa tuhuma mbaya na zenye uongo mwingi na mtu huyo wametendewa haki na mahakama, ambapo “mwanahabari huyo” alikutwa na hatia na kuamriwa kulipa mabilioni ya shilingi kama fidia.

Lengo la makala haya siyo kuongelea kuhusu “mwanahabari huyo” wala unyanyasaji mkubwa aliofanya kwa kila aliyemuona kuwa ni “adui wa Rais Magufuli.” Kadhalika, makala haya haijijangaishi kufahamu endapo “mwanahabari huyo” alifanya uharamia huo kwa maagizo ya utawala husika au ni “kimbelembele” chake tu.

Badala yake makala haya inaongelea tukio moja linaloendelea huko kwenye mtandao wa kijamii wa Twitter, ambapo



Makamba

mtu mmoja ameibuka na tuhuma nzito dhidi ya Waziri wa Nishati, January Makamba.

Ni tuhuma nzito ambazo siwezi kuzitaja hapa kwa sababu nitakuwa namsaidia mtu huyo kusambaza tuhuma hizo potofu.

Naam, ni tuhuma potofu kwa sababu kila anayemfahamu Waziri Makamba anatambua kwamba kiongozi huyo siyo mtu wa kufanya japo asilimia 0.01 - ya anachotuhumiwa na mtu huyo.

Hata hivyo, kinachosikitisha ni ukimya wa vyombo vya dola katika suala hilo. Ni kama vyombo vya dola vinaamini kuwa vikipuuzwa tuhuma hizo, zitapotea zenyewe. Kwa bahati mbaya, mtandao wa intaneti huwa hausahau kitu. Na kupuuzwa tuhuma hakujawahi kuzififisha tuhuma husika.

Lakini pia ni muhimu kwa serikali ya Rais Samia Suluhu ichukue hatua stahiki kuhakikisha haturudishwi zama za yule “mwanaharakati huru” aliyejipa mamlaka ya kuchafua watu wasio na hatia.

Tukurudi zama zile za “mwanaharakati huru” – kwa kushindwa kukemea tuhuma dhidi ya viongozi na hata wananchi wa kawaida, tutakuwa tumeshindwa kuondoa mdudu wa uhasama, hivyo kupandikiza chuki zaidi.

Mwanafalsafa wa Wiki

Usawa sasa upambanue haki

Na Deusedith KAHANGWA

TANGU Azimio la Zanzibar lilipochukua nafasi ya Azimio la Arusha, sababu kuu ya kudai katiba mpya Tanzania ni hoja kwamba katiba ya sasa inatoa mwanya wa kukiukwa kwa “kanuni za mastahili ya kijamii” (principles of justice), kiasi cha kuwafanya baadhi ya raia kufikiri, kuhukumu na kutenda kama watumwa ndani ya nchi yao.

Hivyo, swali la pili kuhusu ‘ujasiriadola’ unaofanyika kupitia mchakato wa katiba mpya kwa ajili ya Tanzania mpya, linapaswa kuwa hili hapa:

“Kama tukichukulia kwamba jamii inayoheshimu “kanuni za stahili” za raia wake ni kikundi cha watu walio chini ya mamlaka moja wakishirikiana kufukuzia maslahi ya pamoja, ambapo maslahi hayo ni hatua ya kwanza katika safari ya kutafuta maslahi binafsi, ushirikiano huo unapaswa kuongozwa na “kanuni za stahili” zenye sura gani?

Profesa Profesa John Rawls (1921-2002) wa Marekani. alijibu swali hili baada ya kuchukua mazuri ya nadharia za stahili (theories of justice) zinazofahamika, na kutupilia mbali upungufu wake.

Nadharia hizo ni pamoja na: ubepari, ujamaa, ulibatariani, uegalitariani, uperisona, uyutilitariani, kanuni ya dhahabu kwa mujibu wa misahafu, na kadhalika.

Kwa mujibu wa jawabu la Rawls, dola ambayo ni “jamii yenye kujali kanuni za stahili inasimamia mgawanyo wa haki na majukumu miongoni mwa wanajamii kwa kuzingatia kaulimbiu ya “kuongeza usawa na kupunguza utofauti” katika jamii. Rawls anaitafsiri kaulimbiu hii kwa njia ya kanuni kadhaa.

Mosi, Rawls anaongelea kanuni ya uhuru sawa kwa raia wote. Kwa mujibu wa kanuni hii, kila mtu anayo haki sawa kuhusu uhuru wa msingi, uhuru ambao kila binadamu anao kwa usawa.

Kanuni hii inasema kwamba, uhuru wa kila raia unapaswa kulindwa dhidi ya



Prof. Rawls

mashambulizi kutoka kwa watu baki.

Hapa kuna uhuru wa kuishi, kufikiri, dhamiri, kuabudu, kupiga kura, kujieleza, kusambaza habari kupitia vyombo vya habari, kutafuta na kumiliki mali binafsi, kukusanyika, kwenda popote bila kuvunja sheria, kutokamatwa kiholela, uhuru wa faragha, uhuru dhidi ya rushwa za uchaguzi, na uhuru dhidi ya ulaghai katika mikataba na matangazo.

Pili, Rawls anaongelea kanuni ya kupunguza makorongo kwenye uwanja wa kisiasa. Kwa mujibu wa kanuni hii, tofauti za kisiasa zinapaswa kupunguzwa kwa kuhakikisha kwamba, mazingira yaliyopo yanajenga uwanja ulio tambarare kwa ajili ya watu wote wanaotaka kugombea nafasi za kiofi katika taasisi za kijamii.

Tupunguze pengo kati ya matajiri na masikini

Kwa mujibu wa kanuni ya uhuru sawa kwa wote, pamoja na kuwa, nafasi za uongozi ni chache kuliko wananchi, bado yanapaswa kujengwa mazingira ambayo yanaondoa ubaguzi holela kwa sababu ya tofauti kama vile rangi, kabila, ukoo, jinsi, dini, eneo la kijiografia anakotoka mtu, na uwezo wa kifedha.

Kwa sababu hii, Rawls anapendekeza kwamba, wakati wa uchaguzi, serikali inapaswa kugharimia kampeni za wagombea wote, kama njia mojawapo ya kujenga uwanja tambarare kwa wagombewa hawa.

Mwanafalsafa wa Wiki

Usawa sasa upambanue haki



Tatu, Rawls anaongelea kanuni ya kupunguza pengo la kiuchumi. Kanuni hii inatamka kuwa, tofauti za kiuchumi zinapaswa kupangiliwa katika namna ambayo inazalisha manufaa makubwa kwa watu wanyonge katika jamii.

Kwa mujibu wa kanuni hii, pamoja na kwamba, mfumo wa kiuchumi unaambatana na tofauti za ujuzi, stadi, kipato, na mali, lakini bado jamii lazima ichukue hatu za makusudi za kuwainua watu wanyonge katika jamii, wakiwemo wagonjwa, walemavu, wazee, watoto, na makundi ya watu yasiyo na nyenzo za uzalishaji.

Kanuni hii inataka watu wenye ujuzi fulani wafanye kazi zinazohusiana na ujuzi huo, bila kujali tofauti holela kama vile za rangi, jinsi, dini, kabila, au eneo la kijiografia.

Pia, kanuni hii inataka kila mtu apate elimu na mafunzo, bila ubaguzi unaotokana na uwezo wa kulipia, ili kwa njia hiyo, watu wote wapate sifa ya kuajiriwa katika kazi na kujipatia mkate wao wa kila siku kutokana na juhudi na maarifa binafsi.

Kwa hiyo, kanuni hii inahimiza kanuni za soko huria katika ajira na uzalishaji; inahimiza uwepeo wa serikali inayotoza

kodi na kuitumia kodi hiyo katika kujenga usawa kwa kutoa huduma za kijamii zinazowanufaisha watu wanyonge.

Huduma hizo ni pamoja na elimu bure hadi chuo kikuu, huduma za afya; miundombinu ya barabara, maji, nishati, na tehama; vyombo vya ulinzi na usalama; na maslahi ya pamoja kama haya.

Chini wa kanuni hii, Rawls anateta "kanuni za stahili" na anazigawa katika makundi manne.

Mosi, kuna "kanuni za stahili" katika mauziano kwa mujibu wa mkataba, yaani "commutative justice."

Pili, kuna "kanuni za stahili" katika kuchangia keki ya taifa kwa kufanya kazi na kulipa kodi stahiki serikalini, yaani "contributive justice."

Tatu, kuna "kanuni za mastahili" katika kugawanya keki ya taifa kupitia huduma za jamii ili kupunguza pengo la maisha kati ya matajiri na maskini, yaani "redistributive justice."

Nne, kuna "kanuni za stahili" katika malipo ya fidia stahiki kwa mtu aliyefanyiwa uonevu na watu, yaani "compensatory justice."

Na tano, kuna "kanuni za stahili" katika kutoa adhabu inayolingana na uonevu alioufanya mtu dhidi ya wenzake, yaani "retributive justice."

Utalii

Semina ya mafunzo kwa waandishi

Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa), Ijumaa Ciliyopita, Aprili 28, kiliandaa semina ya mafunzo kwa waandishi wa habari ambapo walipata mafunzo ya namna ya kuandika habari za kutangaza vivutio vya utalii. Semina hiyo iliyofanyika Hoteli ya Four Points, Dar es Salaam, ilidhaminiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Bodi ya Utalii (TTB) na gazeti la Pambazuko. (Picha zote na Shabani Lulela).



Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania, Damas Mfugale akizungumza na waandishi wa habari katika semina ya mafunzo kuhusu namna nzuri ya kutangaza vivutio vya Tanzania.



Baadhi ya waandishi wa habari walioshiriki katika semina ya mafunzo kuhusu namna bora ya kutangaza vivutio vya Tanzania



Rais wa Chama cha Waandishi wa Habari, Simon Mkina, akihojiwa mara baada ya kukamilika kwa mafunzo.

Tehama itumike kuchechemsha utalii

Na Deusedith KAHANGWA

SEKTA ya utalii inachangia asilimia 17 ya pato la kitaifa nchini Tanzania, na inashika nafasi ya tatu kati ya sekta zinazozalisha ajira kubwa, ikiwa na ajira zinazokadiriwa kufikia 850,000.

Kwa sababu hii, Serikali ya Tanzania imekuwa ikifanya jitihada kuitangaza sekta hii kwa njia mbalimbali, ikiwamo kutumia filamu ya Royal Tour iliyotambulishwa duniani na Rais Samia Suluhu Hassan.

Kutangaza utalii ni kitendo cha kufanya mawasiliano kati ya watalii na mtangazaji wa utalii kuhusu vivutio vya utalii vilivyoko mahali fulani.

Kuna njia nyingi za mawasiliano; baadhi ni njia za kimapokeo kama vile luninga, radio na magazeti yanayochapishwa kwenye karatasi. Na njia za kisasa ni mitandao ya kijamii kama vile Facebook, Twitter, Instagram, Youtube, na Tiktok.

Haya ni majukwaa ya mawasiliano yanayofanya kazi kama mifereji ya habari iliyo sehemu ya mduara wa mawasiliano kati ya mtalii na mtangazaji wa utalii.

Katika mduara huu, taarifa kuhusu utalii ni “ujumbe;” mtangazaji wa utalii kama vile mwandishi wa makala hii ni “mtuma ujumbe”; mtalii anayelengwa ni “mpokea ujumbe”; majukwaa ya mawasiliano yanayotumika kusambaza ujumbe ni pamoja na vyombo vya habari vya kimapokea na pia vya kisasa, hasa mitandao ya kijamii. Vyote hivi ni “mifereji ya habari”; na majibu ya mtalii ni “mrejesho.”

Tofauti kubwa zilizo kati ya vyombo vya habari za kimapokea ni vyombo vya habari mamboleo, yaani mitandao ya kijamii inayotumia kompyuta, ni kama ifuatavyo; mitandao ya kijamii haina mipaka ya kitaifa wala kimabara; inaruhusu watu wengi kuwasiliana



Kompyuta

kwa mpigo bila kufuata ukiritimba wa mifumo ya kiutawala; inayo maandiko yanayofyatuka na kuunganisha kurasa tofauti za kintandao, yaani “hyperlink”; na inaruhusu utengenezaji na utumiaji wa ujumbe “nyumbulifu” yaani “multimedia.”

Ujumbe nyumbulifu ni ujumbe wenye kujumuisha taarifa zenye sura zaidi ya moja kati ya taarifa zenye sura zifuatazo; herufi, tarakimu, herufi-tarakimu, picha, video, na sauti.

Kwa kutuma ujumbe unaunganisha taarifa zenye miundo tofauti ya aina hii, mpokeaji hupata kuelewa haraka. Maana, wahenga husema kuwa, “picha moja ni sawa na maneno elfu moja.”

Kwa hiyo, ni vyema waandishi wa habari kujifunza kutumia mitandao ya kijamii ili waweze kutekeleza majukumu yao makubwa ya kuhabarisha, kuelimisha na kujenga taifa kwa kutumia kalamu zao kuantangaza utalii wa Tanzania duniani.

Kama ilivyo kwa matangazo mengine yoyote, kutangaza utalii ni kitendo cha kutengeneza maudhui yanayoeleza vifurushi vya kiutalii vyenye thamani maalum, na kufanya mawasiliano na watalii tarajiwa.

Mitandao ya kijamii, katika mazingira ya sasa, ndiyo mnjia pekee kuchechemsha taarifa za utalii na vivutio vya Tanzania, hivyo ni vyema ikatiliwa mkazo.

Utalii

Sekta ya utalii kupunguza uhalifu

Na Ada LOVELACE

TAARIFA kwamba sekta ya utalii inazalisha theluthi moja ya ajira zote nchini, inaweza kupewa tafsiri nyingi. Hapa hoja ni kwamba, sekta hii inapunguza uhalifu nchini.

Katika kila jamii inayofahamika, watu wote hugawanyika katika sehemu kuu mbili. Kuna “watiifu wa jamii” na “waasi wa jamii.”

Kwa hiyo, kila taasisi inao mifumo ya kuzuia “uasi wa kijamii” na kuhimiza “utiifu wa kijamii.”

Mifumo hii inagawanyika katika sehemu mbili; kwanza, kuna mifumo ya kielimu inayohimiza ujenzi wa tabia njema, zenye kuwaelimisha watu kuhusu tofauti zilizopo kati ya tunu chanya na tunu hasi, na kisha kuwafanya wapende tunu chanya na kuchukua tunu hasi.

Mtu mwenye tabia inayokubaliana na tunu chanya anakuwa na “tabia njema,” wakati yule mwenye tabia zinazokubaliana na tunu hasi anakuwa na “tabia mbaya.”

Mara nyingi, juhudu za wataalam wa maadili ya kidini zinaoongozwa na nadharia hii, zikiwa zinaimarishwa na dhana ya “uchaji wa kimungu.” Hivyo, wacha Mungu wote ni watu wenye “tabia njema.”

Kwa upande mwingine, tangu mwaka 1968, mwandishi Gary Becker, katika kitabu chake, “Crime and Punishment: An Economic Approach,” alikumbusha dunia jambo moja.

Kwamba, tabia njema inayoambatana na “utiifu wa kijamii” na tabia

mbaya inayoambatana na “uasi wa kijamii, ni mazao ya kanuni za kiuchumi, zinazomruhusu mhusika kupima faida na hasara ya matendo yake, bila kujali historia ya “tabia” yake ya siku za nyuma.

Alichosema Becker (1968) ni kwamba, kila mtu anayo akili na utashi. Hivyo, kila mtu hubainisha na kuchagua malengo, hubainisha na kuchagua mbinu ya kutekeleza malengo hayo, na hubainisha na kuchagua mazingira mwafaka kwa ajili ya utekelezaji wa mbinu hizo; na hatimaye utekelezaji hufuata.

Kwa mfano, kama mtu anaweza kufanya biashara halali na kupata faida kubwa kuliko faida anayoipata kama akifanya biashara ya magendo, basi, mtu huyo ataachana na biashara ya magendo.

Kwa mfano tena, mtu mwenye elimu nzuri, na ajira ya kupata ujira wa shilingi milioni moja kwa mwezi, hawezi kuiba shilingi laki moja, itakayomfanya afungwe miaka saba, wakati katika miaka hiyo saba, angepata mshahara wa jumla ya milioni 84.

Kwa hiyo jamii ikibuni na kutekeleza programu za kiuchumi na kijamii zinazowaongezea vijana fursa zinazowapa sababu ya kuepuka tabia za kihalifu kwa sababu kuna fursa bora zaidi zisizoambatana na uhalifu, uhalifu utapungua.



Wanyamapori ni vivutio vya utalii Wanyamapori ni vivutio vya utalii

Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.



Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au Barua-
Pepe; info@pambazuko.tz

Makala**Utamaduni, mila vivutio vya utalii****Na Renatus CARTESIUS**

MAENE0 hayo manane yanayo sifa moja kuu inayoyauanganisha; Serengeti, Mlima Kilimanjaro, Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere, Hifadhi ya Ngorongoro, Mji Mkongwe Zanzibar, Magofu ya Kilwa Kisiwani, Sanaa ya Miamba ya Kondoa, na eneo la mabaki ya Mifupa ya Dinosa la Tendaguru.

Kwa mujibu wa “Mkatoba wa Kulinda Urithi wa Kiutamaduni na Kiasili Ulimwenguni,” wa mwaka 1972, unaosimamiwa na Umoja wa Mataifa, haya yote ni maeneo yanayofaa kwa ajili ya “utalii wa kiutamaduni na kiasili.”

Kifungu cha kwanza na cha pili vinasema kuwa, neno “eneo la urithi wa kitamaduni na kiasili” linajumuisha mali yoyote ambayo ina “thamani bora ya kidunia” kutokana na sifa za kihistoria, kisanaa, kisayansi, kibinadamu, au uzuri wa kiasili.

Kulingana na tovuti ya Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Elimu (Unesco), kufikia Februari 2023, kulikuwa na vituo 1,154 vya “urithi wa kitamaduni na kiasili” duniani kote.

Tanzania imetia saina Mkatoba wa “Dunia wa Utamaduni na Urithi wa Kiasili” wa 1972. Kwa sasa, Tanzania inayo maeneo manane ya urithi wa dunia kwenye orodha ya Unesco, kama yalivyotajwa hapo juu.

Haya ni maeneo ya kiutalii kwa sababu, kulingana na shirika la Umoja wa Mataifa linaloratibu utalii duniani (UNWTO), utalii ni suala lolote la kijamii, kiutamaduni na kiuchumi ambalo linahusisha watu kuhama kwenda nchi au maeneo nje ya mazingira yao ya kawaida kwa

madhumuni ya kibinafsi, kibiashara au kitaalam.

Watu hawa wanaitwa wageni, ambao wanaweza kuwa watalii au wasafiri, wakazi au wasio wakaaji, na utalii unahusiana na shughuli zao.

Utalii ni sekta yenye angalau aina nane za huduma kwa wageni ambazo ni; malazi, utalii wa matukio na burudani, vivutio, matukio na makongamano, vyakula na vinywaji, huduma za mbalimbali za kiutalii, usafiri, na biashara ya usafiri.

Watalii wanakaribia eneo la utalii kwa sababu ya vipengele vyake vya kuvutia. Kwa hivyo, moja ya sifa kuu za eneo la utalii ni utofauti wa vivutio.

Kwa mtazamo huu, utalii wa kitamaduni ni utalii wa watu unaowawezesha watalii kupata tamaduni halisi zinazochanganya asili, mandhari, ngano, shehehe, ngoma, matambiko, hadithi, sanaa, kazi za mikonono na ukarimu, maeneo ya kuvutia, wanyama wa asili, bidhaa na mazingira ambayo hayapatikani kila sehemu.

Hapa, utamaduni ni ‘kipengele kikuu cha kuvuta’ ambacho huathiri uamuzi wa awali wa mgeni kusafiri hadi sehemu mbalimbali za dunia. Tuutangaze utamaduni wetu.

*Utamaduni chanzo cha kuvuta watalii*

Rais Ruto amtisha Raila

**Na Mwandishi WETU,
Nairobi**

RAIS wa Kenya, William Ruto ameonya Ryeoyote atakayevunja amani ya nchi yake kwa kufanya maandamano kesho, huku akitamka kwamba “mimi ni amiri jeshi mkuu.”

Kauli hiyo ya Rais Ruto inaonyesha “kuchoka” kwa kiongozi huyo kuona serikali yake ikitingwa na maandamano ya kila wiki ambayo yamekuwa yakiiitishwa na kiongozi mkuu wa upinzani, Raila Odinga.

Tangu kukamilika kwa uchaguzi mkuu – mwaka jana ambao ulimuingiza Ruto na chama chake cha Kenya Kwanza madarakani, Raila na wafuasi wake wamekuwa wakipinga ushindi huo na kuhimiza kwamba “alifanya hila na wizi ili kushinda.” Hivyo, kutomtambua kuwa kiongozi wa taifa hilo la Afrika Mashariki.

Raila na wafuasi wake, walipanga kuitisha maandamano makubwa kesho, hasa katika miji mikubwa, ikiongozwa na Nairobi, ili kushinikiza serikali ya Ruto “kuachia ngazi.”

Hata hivyo, Ruto na serikali yake, anapinga kufanyika kwa maandamano zaidi kwa maelezo kwamba yamekuwa chanzo cha vurugu, uvamizi wa biashara na hata vifo, hivyo hayana tija, licha ya kurehusiwa na katiba ya nchi hiyo.

Tayari Mkuu wa Polisi Kaunti ya Nairobi, Adamson Bungei amepiga marufuku maandamano hayo ya chama cha Raila, Azimio.

Akizunguma na waandishi wa habari jana Jumapili, Bungei alisema maandamano yaliyofanyika kwa wiki kadhaa kuanzia Machi, mwaka huu yameashiria kuwepo kwa vurugu na kuhatarisha amani.

Kiongozi huyo wa Polisi aidha alitaja uharibifu wa mali, biashara na maafa yaliyoshuhudiwa kama sababu kuu ya jeshi hilo kuwanyima Azimio fursa kuandamana.

Huku akitambua haki ya kuandamana kikatiba na ruhusa kwa wananchi kuandamana, Bungei alisema



Raila

maandamano ya awali baadhi ya walioshiriki walikuwa na silaha hatari.

Azimio ilikuwa imemwandikia barua, ikiomba kuandamana kesho Jumanne na mkuu huyo wa Polisi Nairobi alitangaza kuzuia kufanyika kwa maandamano hayo.

“Maandamano ya awali yalikumbwa na uhalifu; uharibifu wa mali, biashara na maafa, sasa Polisi haiwezi kuendelea kulea uhalifu kwa jina la maandamano,” alisema.


Akitoa onyo kuhusu watakojaribu kuandamana, Bungei alisema askari wake hawatakuwa tayari kuona amani ikivunjwa, hivyo watatumia sheria kukomesha maandamano.

Kiongozi wa Azimio, Raila aliyerejea Nairobi kutoka ziarani Dubai juzi, alisisitiza kuwa maandamano yao yataendelea kama yalivyopangwa.

Raila aidha alisema upinzani hautalegeza kamba kumchukulia hatua kali za kisheria Inspekta Jenerali Mkuu wa Polisi, Japhet Koome na ‘wengineo’ aliohaji walishiriki kuhujumu upinzani.

“Tumewasilisha majina ya Koome katika Mahakama ya Kimataifa dhidi ya Uhalifu (ICC) huko Hague, hivyo tunasubiri namna sheria za kimataifa zitakavyoamua kutusaidia kuwakamata wahalifu halisi,” alionya Raila.

Raila alisitisha maandamano baada ya Rais Ruto kumrai, akiahidi fursa ya mazungumzo.

Ziara**Rais kazini**

Aprili 27, 2023 - Rais Samia Suluhu Hassan alimuandalia hafla mgeni wake, Rais wa Rwanda, Paul Kagame jijini Dar es Salaam na kualika wageni mbalimbali kwa ajili ya chakula cha jioni. Kagame alikuwa na ziara ya siku mbili. Walioalikwa ni pamoja na viongozi wa dini, wakuu wa vyama shindani na wageni wengine. Picha zinaonyesha waliopata fursa ya kualikwa. (Picha zote na Ikulu).



Baadhi ya mashabiki wa Yanga wakifurahia timu yao kutinga hatua ya nusu fainali.

Na Mwandishi WETU

LICHA ya umeme kukatika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, lakini aibu hiyo huenda ikafichwa kwa furaha ya ushindi kwa timu ya Tanzania, Yanga baada ya kutinga nusu fainali za Kombe la Shirikisho Afrika.

Katika hatua hiyo, tayari Yanga imejihakikishia kupata zawadi inayozidi kidogo Sh. bilioni 1 (\$450,000) kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF). Mshindi wa michuano hiyo atabeba Sh. bilioni 3.

Yanga imetinga hatua hiyo kwa kutoka suluhu; huku ikibeba ushindi wa jumla wa mabao 2-0 ambayo iliyapata huko jiji la Uyo, nchini Naigeria baada ya kuifunga Rivers United.

Kufuatia ushindi huo, ambao ni mara ya kwanza kwa Yanga kufikia hatua hiyo katika michuano ya kimataifa, sasa timu hiyo ya Jangwani, Dar es Salaam, itashuka dimbani kupambana na Marumo Gallants ya Afrika Kusini.

Kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi mara baada ya mchezo, pamoja na kushindwa kuwafunga wapinzani wao, vijana wake wamecheza kwa kiwango kikubwa.

“Vijana wangu wameonyesha kabumbu nzuri, ingawa hatujashinda magoli kama tulivyotarajia, lakini jambo la kufurahisha ni kuwa tumeingia nusu fainali na sasa

kazi ni kwenda kujipanga kwa ajili ya michezo migumu inayofuata,” ameingiza Nabi akizungumza na Pambazuko.

Pamoja na Nabi kusifia vijana wake, lakini safu ya ushambuliaji ya Yanga ilionekana kushindwa kupenya kirahisi ngome ya Rivers, ambayo ilionekana kukamia isifungwe bao.

Katika mchezo huo, Khalid Aucho wa Yanga alipewa adhabu ya kadi ya njano, baada ya mwamuzi kuona alifanya madhambi dhidi ya mchezaji wa Rivers. Pia kadi nyingine ya njano ilitolewa kwa mchezaji wa Rivers, Ohaegbu Sam.

Timu ya Marumo inaingia kuchuana na Yanga katika nusu fainali baada ya jana kuwatoa wapinzani wao kutoka Misri, Pyramid.

Tajiri wa timu hiyo inayoongoza ligi ya Tanzania, Ghalib Said Mohamed ‘GSM’ alitangaza dau la Sh. milioni 300 endapo timu yake itaibuka na ushindi wa idadi yoyote ya mabao.

Hata hivyo, kwa kutoka suluhu haijafahamika endapo GSM itatoa kiasi hicho cha fedha au kuja na uamuzi mwingine kwa Yanga kujihakikishia kushiriki nusu fainali.

Rais Samia Suluhu Hassan alitangaza kuongeza dau kwa kila goli lililokuwa likifungwa na Yanga, kama livyokuwa kwa Simba katika michuano ya soka ya kimataifa.



MSHINDI NI...

Mshindi wa maelezo bora ya picha ya wiki iliyopita ni mwenye nambari 0744 556 747. Tafadhali awasiliane na namba 0754 020 880 ili kupata zawadi yake ya Sh. 10,000. Hongera sana kwake.

Maelezo yake kwa picha: Ni kicheko cha uhakika wa chakula. Ni kicheko cha shukrani. Familia yenye uhakika wa chakula, kama ilivyo kwa taifa, hujaa furaha na faraja, bila kutegemea nguvu za kiuchumi.



Wachezaji wa Timu ya Yanga wakionekana kuomba dua kabla ya kuanza kwa mchezo wao dhidi ya Rivers United kutoka Nigeria. Timu hizo zilichuana jana Dar es Salaam, Tanzania kuwania kutinga nusu fainali za michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika. Pamoja na kutoka suluhu, Yanga ilifanikiwa kuingia nusu fainali kwa jumla ya mabao 2-0. (Picha kutoka mtandao).

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

